**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI).**

**NAMBA ZA SIMU:**
**MKUU WA SHULE 0783087501/0765909626**
**MAKAMU /MKUU WA SHULE 0682914888**
**MATRONI 0682348800**

**SHULE YA SEKONDARI NKUHI**
**MTATURU S.L.P 42**

**MZAZI/MLEZI WA**

**S.L.P……………………..**

**YAH. MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA…………. KATIKA SHULE YA SEKONDARI NKUHI MTATURU ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI MKOA WA SINGIDA MWAKA………….**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha……. katika shule hii mwaka………………na atasoma tahasusi ya PCB/PCM/PGM. Shule ya sekondari Nkuhi Mtaturu ipo umbali wa kilometa 20 kusini mwa Makao Makuu ya Wilaya (Ikungi) Usafiri wa hiace /Coaster kutoka mjini singida unapatikana katika kituo cha mabasi/stendi ya vumbi nauli Tshs 4000/= kwa wale wanaotokea mikoa ya Manyara, Arusha,Tanga, Moshi lakini kwa wale wanaotokea barabara ya DAR ES SALAAM kwa mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya, Katavi, Songea, Ruvuma watashukia Kituo cha NKuhi kabla ya kufika makao makuu ya Wilaya. Kwa barabara kuu inayotoka MWANZA KWENDA DAR ES SALAAM kwa mikoa ya Shinyanga, Kagera, Kigoma, Geita, Mwanza, Simiyu, Mara,Tabora watashukia Kituo cha NKuhi kilometa 50 baada ya kupita Singida mjini.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **itakayotangazwa na Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI**

1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

**1.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni kitambaa chenye Rangi ya Kijani Kibichi. Suruali mbili zenye marinda mawili kwa wavulana, na Sketi Mbili ndefu za Kijani Kibichi rinda Moja mbele na moja nyuma na marinda matatu kwa pembeni.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu
iii. Sare ya Michezo ni track suit 2 za rangi ya kijivu yenye mistari mieupe pembeni na raba pea2
iv. Viatu vya shuleni ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe/nyeusi/khaki za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa wavulana;
vii. Sweta 2 za rangi ya kijani kibichi.
viii. Nguo za kushindia(shambadress)(surua/i ***mbili rangi ya kaki yenye marinda mawili kwa wavulana na sketi za kaki 2 kwa wasichana na track suit rangi ya blue bahari na tisheti ya kijivu)***;
ix. Tai ndefu ya rangi ya kijani kibichi
x. Tisheti(T-shirt) *ya Kijivu panya (formsix), unaweza kuja nayo pia zinapatikana shuleni kwa Tsh*
xi. *15,0001=);*

1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari kaunta Q.4 zisizopungua 15, mathematical set, rula na kalamu za kutosha.
ii. **Ream(A4)**, Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo yatahasusi husika
iv. Godoro lenye upana wa 2.5 futi 6
v. Mashuka Jozi 2 ya rangi ya bluu bahari blanket1, chandarua 1rangi ya bluu (Ni muhimu), mto wenye foronya 1 ya rangi ya bluu

vi. Taulo na nguo za ndani za kutosha;Vyombo vya chakula(sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

vii. Ndoo2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

viii. Kwanja 1**(PCB)**, Jembe 1**(PCM)**, Reki 1**(PGM)**, Mifagio 2 (kwa wote) wa ndani na nje na sabuni ya maji 5L.

**N.B Nguo za nyumbani haziruhusiwi hivyo ni vyema mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule. Mitindo yakunyoa kiduku haukubaliki shuleni kwetu.**

**ANGALIZO**:**Mwanfunzi** atapangiwa kuleta vifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anaosoma

**1.1. Michango mbalimbali**

| NA | AINA YA MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5000/= |
| 3 | Nembo | 5000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hizo za michango zilipwe kwene akaunti ya shule namba 52510010735 yenye jina NKUHI MTATURU SECONDARY SCHOOL benki ya NMB, Mwanafunzia je na Pay in Slip iliyoandikwa jina lake na mchangunuo wake**

2. **Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

3.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni Pamoja na:

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini(90) bila taarifa/utoro
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu au walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, mwanafunzi kumpiga Mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi muda wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi yad awa za kulevya
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xii. Kusababisha mimba
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria ya nchi
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
xv. Kumiliki, kukutwa au ktumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi. Kudharau bendera ya Taifa.
xvii. Kufana jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama vile kunya sumu na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

3.3 **Viambatisho na fomu muhimu**

i. Fomu ya uchunguzi wa afya(Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa serikali
ii. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
iii. Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule na
iv. Picha nne(04) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni, Pamoja na namba zao za simu

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**SULEMAN JUMA ABEIDY**
**KAIMU MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI NKUHI MTATURU**

SHULE **YA SEKONDARI YA NKUHI MTATURU**
FOMU **YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA** SHULE **ALIYOPEWA**

Bandika picha hapa (yenye shati jeupe

**1. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**
- Jina kamili la mwanafunzi. ........................................................................
- Tarehe ya kuzaliwa ............................(ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa)
- Mahali alipozaliwa (Mkoa na Wilaya)
- Uraia: **MTANZANIA/SIYO MTANZANIA**
- Shule uliyotoka ....................................................................................
- Namba ya mtihani (S....................................)

2. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI
- Jina la mzazi/mlezi. ...............................................................................
- Kazi ya mzazi/mlezi ................................................................................
- Anuani ya mzazi/mlezi. ..........................................................................
- Simu ya mzazi/mlezi – kazini ........................... nyumbani.. ......................
Mkononi.. ........................................................... (kama huna nambari ya simu, ya jirani yako) ...................................................................

3. MWANAFUNZI Mimi ........................................ nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule na kujifunza kwa bidii.
Tarehe ...................................... Sahihi. ......................................................

4. MZAZI/MLEZI: Nimehakikisha mwanangu amezisoma na kuzielewa sheria za shule nami nimemsisitiza katika hilo.
Tarehe .....................................
Jina ................................................... Saini ........................................

**NKUHI MTATURU SECONDARY SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINA**

**FROM:**
**The Medical Officer,**
**Government Hospital**
**........................**
**........................**
**........................**

**TO:**
**The headmaster,**
**Nkuhi Mtaturu Secondary School,**
**P. O. Box42**
**SINGIDA.**

**RE: MEDICAL CERTIFICATE**
**(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

I have examined who aspires to join Form I in your school as follows:-

AREA REMARKS........................................

1. Skin ........................................................
2. Eyes ........................................................
3. Ears ........................................................
4. Teeth ........................................................
5. Chest ........................................................
6. Spleen ........................................................
7. Abdomen ........................................................
8. Urine ........................................................
9. Stool ........................................................
10. HB Haemoglobin ........................................................
11. Innoculation againt meningitis ........................................................
12. Sickle cell ........................................................
13. Asthma 14. Any other comments

I consider that he/she* is physically/not physically fit to join your school.

Signature Date

Official stamp

**SHULE YA SEKONDARI NKUHI MTATURU**

Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika Migomo,Fujo na makosa ya Jinai.

(a) Je utashiriki katika mgomo au kushawishi migomo shuleni?

.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.....................................................................................

(b)Je utashiriki katika fujo au kushiriki fujo Shuleni?

.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................

(c)Je utafuata taratibu zote za Shule kama zilivyo?

.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
....................................................................................................

(d) Eleza kwa ufupi juu ya uzalendo wako kwa nchi yako.................................................................................................................

.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
...........................................................................